# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
# CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**015/1 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**

**(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

**Muda: Saa 2** **7 Novemba 2001 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali YOTE.
3. Majibu yako yote yaandikwe katika kijitabu chako cha kujibia.
4. Fuata kwa uangalifu maelekezo ya kila swali.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 7 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Bismillahir-Rahmanir-Rahiim.**

## SEHEMU A (alama 20)
## SUNNAH NA HADITHI

1. Kwa maswali (i) – (x) chagua herufi ya jibu sahihi na kisha andika kando ya namba ya swali katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Sunnah ni mwenendo na mafundisho ya mtume (S.A.W.), wakati Hadithi ni
- A sunnah ya matendoni na vifuani
- B taarifa juu ya Sunnah
- C mapokezi timilifu ya taarifa iliyoletwa na masahaba
- D matendo na Sunnah za taarifa za awali madina za Mtume (S.A.W.)
- E sehemu ya mafundisho ya Qur-an.

(ii) Kwa kuzingatia maana ya Sunnah kisheria, jozi ya matendo ifuatayo ndiyo Sunnah ya Mtume (S.A.W.):
- A Kupanda ngamia wekundu katika msafara wa mapambano na kufuga mbuzi
- B Kuishi Madina katika eneo la msikiti mtukufu na kuomba dua
- C Kuishi kiislamu katika jamii na kuwa mfano
- D Kuwafundisha masahaba na kuwafukuza wageni wasio Waislamu
- E Kutaja jina la Mwenyezi Mungu na kumswalia Mtume.

(iii) Kitu gani kilishamiri zaidi katika kipindi cha Tabii Tabiin?
- A Uandishi wa hadithi zote za Mtume na masahaba
- B Kumuigiza Mtume (S.A.W.) katika medani ya mapambano
- C Uandishi wa hadithi sahihi
- D Msururu wa wapokezi na waandishi mashuhuri kuhamia Basra
- E Kuikusanya na kuihifadhi Qur-an

(iv) Waislamu kama jamii watanufaika na Sunnah ya Mtume (S.A.W.), kama
- A wote watafunga Jumatatu na Alhamisi na kupiga kura Kiislamu
- B wataitangaza Sunna ya Mtume (S.A.W.) kwenye makongamano
- C watasoma visa vya masahaba waliomuona Mtume (S.A.W.) na kufanya naye kazi pamoja
- D wataanzisha mashindano ya hadithi kila mwaka na kuzishirikisha katika hilo madrasa za mijini tu
- E wataifanya Sunnah ya Mtume (S.A.W.) ndiyo dira ya kuitafsiri Quran katika matendo.

(v) Alqatadaya ni kitabu mashuhuri cha hadhithi kilichoandikwa katika kipindi cha
- A Tabiin
- B nusu karne kabla ya kutawafu Mtume (S.A.W.)
- C Makhalifa na watu wema wote
- D Makhalifa wanne waongofu
- E baada ya Makhalifa wanne.

(vi) Kimoja kati ya vifuatavyo ni kigezo sahihi cha hadithi:
- A Isnad yake isikamilike kwa maneno ya maswahaba tu
- B Isnad yake isitoe maelekezo yaliyokusudiwa
- C Isipingane na Quran
- D Isichukuliwe nzima nzima, bila ya kupata baraka za Makhalifa waongofu
- E Ikubalike na jamii husika.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(vii) Al-Muwatta ni kitabu mashuhuri cha hadhithi kilichoandikwa katika kipindi cha
- A Masahaba waongofu
- B Tabiin
- C Tabii Tabiin
- D kuporomoka kwa dola na kuibuka kwa waandishi
- E maimamu wakuu.

(viii) Mwandshi mashuhuri wa hadithi katika kipindi cha Tabiin alikuwa nani?
- A Imam Abu Daud bin Anas Malik
- B Imam Muslim wa Tirmidhi
- C Imam Maliki bin Adnan
- D Imam Maliki bin Anas
- E Imam Shafi

(ix) Msururu wa wapokezi tokea aliyemuona au kumsikia Mtume (S.A.W.) hadi kufikia mwandishi aliyeipokea na kuiandika hadithi ni
- A Isnadul – Maarifa
- B Matin sahihi
- C Isnad
- D Matin Isnad na Bukhar Muslim
- E Isnad-Maarifa.

(x) Kutokana na taarifa kutoka kwa masahaba juu ya mwenendo wa Mtume (S.A.W.), waislamu wa leo wanaweza kujua
- A Sunnah ya Mtume (S.A.W.)
- B Jinsi hadithi za Mtume (S.A.W.) zilivyokusanywa
- C Maadui wakuu wa harakati zilizopelekea Mtume (S.A.W.) kuhamia Basra na Yathrib
- D Vitabu mashuhuri vya hadithi na mafundisho yake
- E Watu wema waliomsaidia Mtume (S.A.W.).

## SEHEMU B: (alama 20)
## QURAN

2. Chagua kutoka orodha B kifungu kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka orodha A.

### ORODHA A

- (i) Quran ni neno la Allah (S.W.)
- (ii) Hoja za makafiri dhidi ya Quran
- (iii) Ushahidi wa kuwepo karatasi wakati wa Mtume (S.A.W.)
- (iv) Quran haitabadilishwa
- (v) Kuwepo kwa akhera
- (vi) Njia za mawasiliano na Mwenyezi Mungu
- (vii) Uteremsho wa kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu, mwenye hekima (39:1)
- (viii) Itakapofika nusura ya Mwenyezi Mungu na kushinda na kuwaona watu wanaoingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi kwa makundi ……. (110: 1-3)
- (ix) Kuhifadhiwa kwa Qur-an
- (x) Hoja zitakazowapelekea watu kwenda motoni

### ORODHA B

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

A "Wala usiutikise ulimi wako kuufanyia haraka wahy ............. .." (75:16)
B Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba (96:1)
C "Na kwa kitabu kilichoandikwa kwenye karatasi na kikakunjuliwa" (52:2-3).
D Bibi Aisha (r.a) amesema "kilichoanza katika wahy wa Mtume (S.A.W.) ni ndoto za kweli. Alikuwa Mtume (S.A.W.) haoti chochote isipokuwa kilitokea kana alivyoota ............. " (Bukhari).
E Quran ni visa vya watu wa kale (53:13) na ni hadithi tu za watu wakale. (6:25)
F "Basi ni lipi likupalo kukadhibisha malipo? ( 95:8)
G "Uteremsho wa kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu, mwenye hekima" (45:2).
H Lakini makafiri walisema "Hayo anayo simulia (Muhammad) ni ndoto zilizovurugika, bali anayabuni mwenyewe, bali huyu ni mtunga mashairi tu .........." (21:5).
I "Na haikuwa kwa mtu kwamba Mwenyezi Mungu anasema naye ila kwa ilhamu au kwa nyuma ya pazia au humtuma mjumbe ...........(42:51)
J "Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia mtume wetu, basi leteni sura moja iliyo mfano wake na muwaite waungu wenu bighairi ya Mwenyezi Mungu ikiwa mna kweli" (2:23).
K "Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizopewa mlizitumiaje)" (1..8)
L "Haitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na mwenye hekima ahimidiwaye" (41:42).
M "Na bila shaka tunajua kwamba wanasema yuko mtu anayemfundisha" (16:103)
N "Hawaizingatii nini, hii Quran? Na kama ingelitoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangekuta ndani yake khitilafu nyingi" (4:82)
O Hakika sisi ndio tuliyoteremsha mawaidha haya na hakika sisi ndio tutakaoyalinda" (15:9)
P Uthman bin Affan (r.a) anasema "wakati wowote mtume wa Allah (S.W.) alipoteremshiwa wahy humuita mmoja wa watu waliochaguliwa kuandika". (Tirmidh).
Q "Na Mola wako atakupa mpaka uridhike"
R "Wewe huna lako katika shauri hili (ni juu ya Mwenyezi Mungu) awasamehe au awaadhibu maana wao ni madhalimu" (3: 128)
S "Wale wanaokula riba hawasimami ...... hali Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na kuharamisha riba ......." (2: 275)
T "Kumekughafilisheni kutafuta wingi (wa mali, watoto , vyeo nk.) hata mmeingia makaburini" (102: 1 – 2)

## SEHEMU C (alama 20)
## TAUHID

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki.

(a) (i) Kuamini Malaika
(ii) Kuamini Mwenyezi Mungu
(iii) Kuamini siku ya mwisho na Qadar
(iv) Kuamini mitume
(v) Kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu

(b) (i) Tumeamini
(ii) Walisema wanaokaa jangwani
(iii) Sema (uwaambie) hamjaamini (kweli kweli bado)
(iv) Maana imani haijaingia vyema nyoyoni mwenu
(v) Lakini semeni tumesilimu
(sehemu ya aya ya 14 ya sura ya 49)

(c) (i) Bila shaka wewe ni mwenye uweza juu ya kila kitu.
(ii) Kheri imo mkononi mwako.


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(iii) Sema, Ewe Mola uliyemiliki ufalme wote
(iv) Na humtukuza umtakaye na humdhalilisha umtakaye
(v) Humpa ufalme umtakaye na kumuondolea ufalme umtakaye (3:26)

## SEHEMU D (alama 20)
## FIQH

4. Jibu kwa ufupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika maswali (i ) - (xv) . Andika neno au maneno yanayokosekana tu, katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Makundi mawili ya Figh ni ____________ na ____________________
(ii) Kwa mujibu wa Uislamu, nafasi ya mwanadamu hapa ulimwenguni imetukuzwa kwa kuwa ni ________________ wa ____________________.
(iii) Makafiri na washirikina wameidunisha nafsi ya mwanadamu hapa duniani kwa kumfanya ni ________________ na ______________ au mfungwa wa mahitaji yake.
(iv) Ibada au kuabudu katika Uislamu ni kuishi maisha ya kufuata ________________ ya Mwenyezi Mungu na kujiepusha na ______________ yake.
(v) Lengo kuu la nguzo za Uislamu ni kutoa mafunzo yatakayomwezesha mja kuishi maisha ya ________________, ____________________.
(vi) Faradhi za udhu ni kuosha uso, mikono, miguu, kupaka kichwa ____________ na ________________.
(vii) Swala za Faradhi zimegawanyika makundi makubwa mawili. Faradhi ___________ na Faradhi ________________.
(viii) Sijda sah'u huletwa kwa kusahau, kuongeza au kupunguza ________________ au ___________ za swala.
(ix) Andika tafsiri ya aya ya Quran inayo bainisha lengo la zakat.
(x) Mambo yanayofunguza swaumu ni kujamiiana ________ na ________________.
(xi) Tofauti kubwa katika fikra ya mamlaka katika mfumo wa siasa wa Kiislamu na Kitwaghut, ni kuwa katika Uislamu (power) mamlaka ni ya ___________ wakati katika Utwaghuti mamlaka ni ya ____________________.
(xii) Mfumo wa uchumi wa Kitwaghuti upo kupata ____________ wakati ule wa kiislamu unazingatia ______________ watu.
(xiii) Moja ya kasoro kubwa ya sheria ya ndoa ya mwaka ______________ ambayo inapingana na Uislamu ni mahakama kupewa kazi ya kutoa ____________________.
(xiv) Katika Umra au Hija Tawafu inafuatiwa na tendo la ________________ na ________________.
(xv) Njia kuu tatu zinazowapotosha Waislamu katika maisha yao ya kila siku ni utii kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kuifuata ______________ na kuwatii ______________.

## SEHEMU E (alama 20)
## TAREKH

5. Chagua neno au kifungu cha maneno (i) – (xxxii) ili ukamilishe kauli (a) – (p) kwa usahihi.

### MANENO/VIFUNGU VYA MANENO

(i) Uislamu
(ii) Dini
(iii) Uhai
(iv) Mwaminifu
(v) Kisiasa
(vi) Utume
(vii) Hira
(viii) Mwenyezi Mungu



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(xi) Quran
(xii) Mkwawa
(xiii) Elimu
(xiv) Uongozi
(xv) Hudaibiya
(xvi) Zimis
(xvii) Umoja
(xviii) Kufa
(xix) Mkweli
(xx) Swala
(xxi) Kufaradhishwa swala
(xxii) Kiuchumi
(xxiii) Katiba
(xxiv) Kuu
(xxv) Imani
(xxvi) Ummah
(xxvii) Majimbo
(xxviii) Kuoneshwa alama za Mwenyezi Mungu
(xxix) Wayahudi
(xxx) Sunnah
(xxxi) Majimaji
(xxxii) Makkah

(a) ______________________ ndiyo __________________ iliyofunzwa na Mitume wote.

(b) Sayansi imethibitisha leo kuwa bahati nasibu haiwezi kuleta ________________ hivyo mwanaadamu anabaki kiumbe wa__________________________.

(c) Mambo mawili maarufu yanayoonesha kuwa mitume hawaathiriwi na mazingira katika maisha ya kabla ya kupewa utume kwa Mtume Muhammad (S.A.W.) ni ______________________ na ______________________

(d) Wingi wa huruma na kuchukia maovu yaliyokuwa yakifanywa katika jamii yake, kumempelekea Mtume kuishi maisha ya upweke (kujitenga) katika Jabal ______________________ na ambako huko huko ndiko alikopewa ___________________.

(e) Makafiri wa Makkah walimpinga Mtume na utume wake kwa sababu za ________________ na ____________________________.

(f) Mateso waliyofanyiwa waislamu wa Makkah na makafiri wa Kikureishi hayakuteteresha bali yaliwaongezea _____________ na kuwa tayari ________________ kuliko kuacha Uislamu.

(g) Amri mbili za kwanza alizopewa Mtume (S.A.W.) ambazo ni nguzo za kusimamisha Uislamu ni ________________________ na ________________________.

(h) Sababu mbili za msingi zilizofanya mtume apelekwe Israa na Miiraj ni ______________________ na ____________________________________

(i) Taasisi za kisiasa alizoanzisha Mtume (S.A.W.) huko Madina ambazo zilisaidia kuanzisha serikali ya Kiislamu ni msikiti na ____________________, Shoura na ________________.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(j) Katika kuendesha serikali ya Kiislamu Mtume alianzisha serikali ____________________ na serikali ya ____________________.

(k) Serikali huwa ya Kiislamu pale inapoendeshwa kwa misingi ya ____________________ na ____________________.

(l) Mkataba wa ____________________ ndio uliounda hali iliyopelekea kukombolewa kwa _______________ na ushindi wa Uislamu.

(m) Wapinzani wa Dola ya Kiislamu walikuwa Makafiri wa Kikureishi na wasaidizi wao, wanafiki, _______________ na ____________________.

(n) Bila ya mchango wa Waislamu kupigana Jihadi na Wajerumani katika vita vya ____________________ pwani na vita vya ____________________ Iringa, uhuru wa nchi hii ungechelewa zaidi.

(o) Makafiri katika Dola ya Kiislamu huitwa _______________ na hutakiwa kulipa kodi ya _______________.

(p) Mambo mawili makubwa miongoni mwa Waislamu yanayowamisha maendeleo ya Uislamu ni ____________________ na ____________________.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org